Barabara ya Tanzania
Kwenda Damascus

Ludovick S Mwijage

Mustakabali wa Taifa

Hali ya Katiba ya Tanganyika, 1961—1962

Mataifa, yakiwemo yaliyo chini ya mifumo ya kiimla, yana Katiba zake. Lakini katika taifa lenye demokrasia ya kweli; kama Tanganyika ilivyokuwa kuanzia 1961 hadi 1962; Katiba hufafanua madaraka ya kisiasa na wajibu wa raia kwa taifa lake. Katiba pia hufafanua chanzo cha madaraka hayo; uhalali wa wanasiasa kuyatumia madaraka hayo, na jinsi madaraka yenyewe yaliyvo sambazwa kwenye mihimili mitatu ya dola.

Mihimili hii ni Bunge, Mahakama, Utawala; na kwa kiasi fulani wananchi wenyewe kutokana na uwezo walionao kuamua nani awe mwakilishi wao, au aliongoze taifa. Lakini pia kuna mhimili mwingine muhimu unaovihusisha vyombo vya habari. Huu hufahamika kama Mhimili wa Nne (Fourth Estate).

Mihimili mitatu iliyotajwa mwanzo hutegemeana kwa kiasi fulani kwa sababu yote ni sehemu ya viungo vya serikali yenyewe. Hata hivyo, uhuru wa mihimili hii kutoingiliwa kiholela na Utawala ndio msingi mkuu wa demokrasia ya kweli.

Mojawapo ya kazi muhimu ya Mhimili wa Nne ni kutaarifu umma mambo ambayo serikali inapashwa kuyafanya lakini haiyafanyi. Kadhalika, mhimili huu huwajulisha wananchi maendeleo serikali iliyoyaleta; uhusiano wake na mataifa ya nje, na mengineyo.

Kwa hiyo, huu pia ni mhimili muhimu sana katika kuimarisha demokrasia na kukuza utamaduni wa serikali kuwajibika kwa wananchi wake.

Ndiyo kusema, ni mihimili hii **iliyo huru** ambayo kwa pamoja hufanya demokrasia iwezekane katika jamii ya kisiasa. Mifumo mingine iliyo nje ya utaratibu huu, haikidhi kanuni za demokrasia ya kweli.

Katiba ya nchi yaweza kuwa imeandikwa au haikuandikwa kama vile za New Zealand, Israel na United Kingdom. Katika mataifa mengi, Katiba iliyoandikwa ni ngumu kuirekebisha bila kufuata utaratibu maalum. Mathlan, tangu itangaze uhuru wake tarehe 4 Julai 1776, Marekani imefanya jumla ya marekebisho 27 tu katika Katiba yake.

Lakini Katiba ambayo haikuandikwa inaweza kurekebishwa kwa urahisi (kama ambavyo hufuka) ili kukabiliana na hali mpya. Makala haya yanazungumzia tu Katiba ya kidemokrasia iliyoandikwa.

Watunzi wa Katiba hii sharti wazingatie baadhi ya vipengele vya Mkataba wa Umoja wa Mataifa vinavyolenga kuhami haki za binadamu na utukufu wa mtu. Haki hizi zinachukuliwa kuwa za lazima sana kwa kila binadamu kiasi kwamba ulinzi wake ni jukumu la jamii nzima ya kimataifa.

Inafuatia kwamba, ingawa taifa-hali linaweza kuamuru manispaa ya sheria, katika mazingira fulani, linaweza lishindwe kutekeleza sheria hiyo kama inapingana na kanuni za Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu haki za binadamu.

Mkataba wa Umoja wa Mataifa ulitokana na mkutano uliofanyika tarehe 26 Juni 1945, mjini San Francisco, Marekani. Wawakilishi wa mataifa yaliyo saini Mkataba huo pia waliweka saini kwenye hati nyingine maalum iliyokuwa na vipengele kadhaa vinavyohusu haki hizi. (Tanganyika iliridhia Mkataba huo ilipojiunga na shirika hilo tarehe 14 Desemba 1961 na Zanzibar ilifanya hivyo tarehe 16 Desemba 1963).

Kifungu cha 62(2) cha Mkataba wa Umoja wa Mataifa kinaipa Kamati ya Uchumi na Huduma za Jamii ya shirika hilo jukumu na madaraka, kuhakikisha kwamba mataifa yanazilinda haki hizi. Zipo mamlaka nyingine chini ya mwavuli wa Umoja wa Mataifa, zinazofuatilia kwa makini uvunjwaji wake.

Baadhi ya mamlaka hizi ni Umoja wa Mataifa kwa Ajili ya Haki za Binadamu; Umoja wa Mataifa Juu ya Mateso Mwandishi Maalum na Mahakama ya Kimataifa ya Jinai. Mahakama hii huwaleta mbele ya sheria wahalifu wa vita; wa haki za binadamu na wengine waliotenda uhalifu mwingine dhidi ya mtu.

Haki za binadamu na demokrasia havitenganishwi kwa maana hufurahiwa sanjari; na, kwa hiyo, ni vigumu jamii ya kimataifa kuzitetea haki za binadamu lakini pia bila kuitetea demokrasia ya kweli.

Na ingawa Umoja wa Mataifa ni shirika lisilokuwa na vyombo vyake vya kukazia maazimio na kanuni zake linaweza, kupitia Kamati ya Usalama ya shirika hilo, kuyaomba mataifa yenye uwezo huo kuchukua hatua madhubuti ili kuthibiti uvunjwaji wa haki za binadamu uliokithiri; au kama kupuuzwa kwa demokrasia kunaweza kuwa na madhara nje ya mipaka ya taifa-husika.

Yote haya yanaonyesha haja ya watunzi wa Katiba ya nchi kuvizingatia vipengele hivi; na viongozi wa kisiasa kuzingatia utawala wa sheria siyo tu kwa kuwa uimla na utawala wa kibabe havikubaliki, bali pia kuipa demokrasia nafasi kuimarika kama msingi wa taifa changa. Kwa maana, taifa changa likijengwa kwenye msingi wa utawala wa kiimla linaweza kuzorota sana kimaendeleo.

Sababu yenyewe ni kwamba, uhai wa utawala huu kama mfumo wa serikali, hutegemea hofu aliyonayo mtawaliwa pamoja na udhaifu wake kiuchumi. Wananchi wakiwa katika mseto wa hali ya namna hii, ni rutuba nzuri utawala wa kiimla kushamiri.

Kwa mfano, kila kukicha wananchi sharti wafikirie namna ya kuweka mlo mezani; wapige bongo wapi, na namna gani, watasaka mahitaji mengine muhimu kwa ajili ya familia zao, na mengineyo. Hofu na mapambano ya kila siku dhidi ya ugumu wa maisha haviwapi wananchi fursa ya kutosha kufikiri na kuhoji mtawala anafanya nini.

Lakini ni tabia ya kutowajibika ambayo hujenga utamaduni wa kiburi ambacho humfanya mtawala kutumia madaraka kufanya anachopenda. Warithi wa kisiasa wa mtawala huyu wakikabidhiwa madaraka bila kuwajibika kama yeye, huweza kuyatumia vibaya pengine kuliko hata yeye. Wakati mwingine siyo ajabu wayatumie madaraka hayo kujilimbikizia mali; mali ambayo huimarisha nguvu zao za kisiasa na kiuchumi katika jamii.

Na kadri ambavyo tabaka-tawala huzidi kujilimbikizia mali na kutunga sheria za kuhami maslahi yao, tahayuri kwa raia wa kawaida mtaani pia hukithiri. Mwishoni, raia wa kawaida hujikuta amekwama kwenye mzunguko huo miaka nenda rudi.

Chukua mfano wa Haiti. Tangu tarehe 1 Januari 1804 wakati raia (weusi) wa taifa hilo walipo jinasua kutoka mfumo wa utumwa na kutangaza uhuru wao, hawajaweza kuimarisha usalama wa taifa lao na kujiinua kiuchumi.

Badala yake, pamoja na kwamba Haiti ni taifa dogo na lenye idadi ndogo ya watu, 'maendeleo' yanayoonekana nchini humo ni kuwepo makundi ya kihalifu yanayoshindana. Aidha, yapo 'maendeleo' ya watu wenye 'ubunifu' wa mbinu mpya za uhalifu, kama njia ya kujipatia riziki. Dhahiri, wapo raia wema lakini maisha yao hayana tofauti na hali iliyokwisha zungumziwa hapo juu. Kusugua chumvi katika jeraha, taifa lote kwa ujumla huamini katika dini tata ya vodou (syncretic religion).

Haistajabishi, kwa maana mwanadamu akipoteza imani katika nafsi yake, kinachobaki ni ombwe. Katika mazingira magumu kama hayo, ni rahisi sana ombwe kujazwa na imani tata—nje kabisa ya imani za kawaida.

Kwa hiyo, kukosekana maendeleo nchini Haiti licha ya zaidi ya miaka 200 tangu nchi hiyo ijitawale ni mfano mmoja, kati ya mingine mingi, unaoonyesha kwamba utawala wa kiimla siyo msingi bora wa kulijenga taifa changa.

Linganisha tena mataifa ya Magharibi na Mashariki; au tazama kiwango cha umaskini (na makovu ya kisaikolojia) katika mataifa ya Ulaya Magharibi ambayo hadi miaka ya 1970 yalikuwa chini ya utawala wa kiimla.

Ni kweli, haki za binadamu na demokrasia peke yake haviweki mlo mezani; lakini hujenga utamaduni wa uwajibikaji, na kuzuia tabaka-tawala kutojinufaisha visivyo halali—na kwa gharama ya mlipa kodi maskini. Kurithishana madaraka, upendeleo pamoja na uswaiba wa kisiasa siyo sehemu ya demokrasia ya kweli.

Ndiyo kusema, katika mataifa ambapo raia wake wana uwezo mzuri zaidi wa kuweka mlo mezani, waliyazingatia mambo haya tangu mwanzo kama maadili ya msingi kwa mataifa yao.

Wapo watakaodai kwamba nchi kama China, isiyokuwa na demokrasia, imesonga mbele mno kiuchumi (japo kwa gharama kubwa ya haki zinazozungumziwa), hadi kuwa taifa lenye nguvu duniani. Lakini huu ni mfano uliojitenga.

Kwa maana, uimla wa kitaasisi ni tofauti kabisa na uimla wa mtu binafsi. Chini ya uimla wa kitaasisi, ni rahisi sana taasisi yenyewe kumuondoa mtawala mbovu madarakani. Mathlan, Mao

Zedong, muasisi wa mapinduzi ya China, alipoaga dunia tarehe 9 Septemba 1976 akiwa na umri wa miaka 82, alimchagua Hua Kuo-Feng (pia hujulikana kama Su Zhu) kuliongoza taifa la China.

Lakini Kamati Kuu ya chama cha Kikomunisti iliyokaa kutoka tarehe 18 hadi 23, mwezi wa Agusti 1980, ilifikia uamuzi kwamba Hua Kuo-Feng avuliwe nyadhifa zote alizokuwa nazo kitaifa, kwa kuwa alionekana hafai. Ingawa sababu za kuondolewa kwake madarakani ni gumzo linaloendelea miongoni mwa wanahistoria, kwamba aliondolewa na taasisi (chama-tawala) ni uthibitisho kwamba ni taasisi hiyo iliyokuwa na madaraka na wala siyo Hua Kuo-Feng binafsi.

Lakini chini ya utawala binafsi siyo rahisi kumuondoa mtawala madarakani; kwa maana utawala wa namna hii msingi wake ni utu-ibada (personality cult). Hali hii inaweza kueleza tofauti baina ya Korea ya Kaskazini, kwa mfano, na Jamhuri ya Watu wa China yenyewe.

Kwa kifupi, taifa kujengeka au kutojengeka hulingana na msingi viongozi wa mwanzo waliouweka pamoja na mpangilio wa Katiba yenyewe.

Katiba ya kidemokrasia siyo lazima iwe na Muswada wa Haki (Bill of Rights). Sababu yenyewe ni kwamba, haki zilizomo kwenye Muswada huo hulindwa moja kwa moja na Amri ya Sheria na Sheria ya Kawaida.

Ndiyo kusema, ingawaje Katiba ya Tanganyika ya 1961—1962 haikuwa na Muswada wa Haki, haki za binadamu zilitambuliwa na kuhakikishwa na sheria iliyopokelewa (received law), na kwenye utangulizi (preamble) wa Katiba yenyewe.

Isitoshe, mtu angeliweza kutumia Mapitio ya Mahakama kwa lengo la kutazama upya uamuzi wa rasmi ya umma; kama uamuzi huo ni tata; ili mradi mlalamikaji awe anaguswa na uamuzi wenyewe.

Kadhalika, chini ya mfumo huu, viongozi wanaoiendesha Katiba huwa chini ya sheria na wala siyo juu yake.

Kinga ya Katiba (sovereign immunity) inamhami kiongozi dhidi ya makosa ya kiutendaji; yasiyokuwa na uovu uliofikiriwa kabla; na wala siyo makosa yanayohusu uvunjwaji wa haki za binadamu, au matumizi ya jinai ya madaraka ya kisiasa na nguvu za dola.

Kulingana na mpangilio huu, serikali huwajibika moja kwa moja kwa Bunge. Kiongozi wa chama chenye viti vingi bungeni ndiye anayepashwa kuunda serikali. Baraza la Mawaziri hutokana na wabunge wa chama hicho, wanao wakilisha majimbo yao.

Kwa hiyo, Baraza la Mawaziri likitokana na wabunge waliochaguliwa moja kwa moja na wananchi, inapatikana serikali inayotokana na mpiga kura. Serikali ya namna hii ina uwezo mzuri zaidi wa kuboresha hali ya mpiga kura.

Sababu yenyewe ni kuwepo aina ya mkataba kati ya mpiga kura na mpigiwa kura: boresha hali ya mpiga kura ili mpiga kura aendelee kukupa kura yake.

Ndiyo kusema, serikali ikishindwa kuzitimiza sera ilizozinadi kwa wananchi wakati wa kampeni za uchaguzi, wananchi wanaweza kuiondoa serikali hiyo madarakani kwa kutumia utaratibu ulioileta madarakani.

Aidha, baada ya kuchukua madaraka serikali haiwezi kutekeleza sera tofauti na zile ilizozinadi kwa wananchi wakati wa kampeni za uchaguzi. Serikali ikifanya hivi huwa imekiuka misingi ya demokrasia, na inaweza kuchukuliwa hatua zinazoelezwa ndani ya Katiba yenyewe.

Kwa maana, wananchi watakuwa wamekichagua chama kushika madaraka siyo kwa sera ambazo viongozi wa chama hawakuzisema, bali kwa kuvutiwa na sera za chama hicho—kama viongozi wa chama walivyozinadi kwa wananchi wakati wa kampeni za uchaguzi. Itikadi ya chama pia hufuata mkondo huo.

Itikadi ya chama sharti ifahamike wakati chama kinapoundwa na wala siyo baada ya chama kuchukua madaraka. Kwa mfano, kundi la watu wenye mlengo mmoja wa kisiasa linaweza kuunda chama cha kisoshalisti, kiliberali, au cha mhafidhini. Kwa hiyo, hata kama wananchi wangelichagua mojawapo ya vyama hivi kwa sababu nyingine zisizo za kiitikadi, watakuwa wanaifahamu itikadi ya chama walichokileta madarakani.

Kadhalika, chini ya Katiba hii, kiongozi wa nchi (head of state) huwa hana madaraka ya kiutendaji. Madaraka yake huwa ni taadhima ya ofisi yake ambayo ni taasisi muhimu katika kuhifadhi mshikamano wa taifa.

Kiongozi wa Baraza la Mawaziri (Waziri Mkuu) hufahamika kama wa kwanza katika Baraza la Mawaziri. Maana yake ni kwamba, Waziri Mkuu ni sawa na mawaziri wenzake, ila tu yeye ni wa kwanza. Hii ndiyo sababu yeye, pamoja na mawaziri wenzake, huitana kwa majina yao ya mwanzo badala ya kuitana kwa vyeo, au majina yao ya mwisho. Hawalazimishwi kufanya hivi, bali ni utamaduni uliofuka chini ya mfumo huu.

Ndiyo kusema, ni kwa nadra sana mtu mmoja kujitafutia sifa kwa gharama ya wenzake; au tuseme Waziri Mkuu kujing'arisha kwa kujizungusha na kundi la mawaziri wasiong'ara kama yeye—na kwa gharama ya maendeleo ya taifa.

Isitoshe, Baraza la Mawaziri hufanya kazi kama timu na maamuzi yaliyochukuliwa huwajumuisha wote. Hii ndiyo kanuni ya serikali kuwajibika pamoja. Waziri asiyekubaliana na uamuzi wa Baraza hilo, sharti ajiuzuru ili aweze kuupinga uamuzi huo akiwa nje ya serikali.

Vinginevyo, kama tulivyoona tangu mwanzo, suala la 'kofia mbili' (multiple powers) halijitokezi. Hii inamaanisha kwamba, chini ya mfumo huu, haitokei kiongozi wa serikali awe tena ndiye kiongozi wa nchi (head of state).

Lord John Emerich Edward Dalberg Acton wa Uingereza (1834—1902) alionya juu ya uwezekano wa madaraka kuzaa ufisadi wa kimadaraka—hasa madaraka yasiyokuwa na kikomo. Kwa hiyo, ufisadi wa kimadaraka aliouzungumzia Lord Acton unapunguzwa kwa kiasi kikubwa, kwa kuyatenga madaraka yenyewe: 'Kheri kukinga kuliko kutibu'.

Kwa kifupi, mfumo wa Katiba hii ulikwisha tumiwa (na unaendelea kutumiwa) na mataifa mengi ya Jamii ya Madola na kuonekana kwamba unayo mizani (checks and balances) ya kidemokrasia.

Mizani hii inahitajika ndani ya mfumo wa serikali ili kujaribu kumzuia mtawala asishawishike kuyanyakua madaraka ya dola (sovereign authority). Kama mtawala anaweza kufanikiwa kufanya hivi, matokeo huwa ni sawa na hayo yaliyokwisha kuzungumziwa mwanzo i.e. utawala binafsi kama siyo utu-ibada.

Tanganyika iliutumia mfumo huu kutoka Oktoba 1960, wakati Bwana Julius Kambarage Nyerere alipokuwa akiiongoza serikali ya mseto kama Waziri Kiongozi (Chief Minister).

Kadhalika, tangu tarehe 1 Mei 1961, wakati Bwana Nyerere alipochukua ofisi ya Waziri Mkuu (Prime Minister), Tanganyika iliendelea na mfumo huu. Hazipo kumbukumbu zinazoonyesha kama wakati wa vipindi hivi viwili serikali ilikumbana na vikwazo kutokana na mfumo wenyewe.

Ilikuwa tarehe 9 Desemba 1961 Tanganyika ilipopata uhuru kamili. Siku mbili baadaye, tarehe 11 Desemba 1961, Prince Phillip, mme wa Malkia wa United Kingdom, alilfungua kikao cha kwanza cha Bunge la Tanganyika.

Katika hotuba aliyoitoa Bungeni kwa niaba ya serikali, Prince Phillip alisema kwamba serikali ya Bwana Nyerere ingelizingatia mambo matatu muhimu katika utekelezaji wa siasa yake ya mambo ya nchi za nje. Alisema la kwanza kati ya mambo hayo, ingelikuwa uzingatiaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa.

'Uzingatiaji' huo ulimaanisha kuilinda Katiba ya kidemokrasia iliyokuwa imetungwa kwa kuzitilia maanani kanuni za shirika hilo. Siyo hilo tu, bali ni Katiba hiyo iliyoileta serikali ya T.A.N.U madarakani na ambayo kiongozi wa chama hicho aliapa kuilinda wakati alipochukua madaraka.

****

Kuangushwa Katiba ya 1961—1962

Kama ilivyoangushwa serikali ya Zanzibar tarehe 12 Januari 1964; siku 33 baada ya kupata uhuru tarehe 10 Desemba 1963; Katiba ya Tanganyika nayo iliangushwa mapema mno, wakati baadhi ya wananchi wakiwa wanaendelea na sherehe za uhuru.

Tarehe 31 Mei 1962 serikali iliwakilisha muswada bungeni (Bunge lilikuwa na wabunge wengi wa T.A.N.U) ikitaka uanzishwe mfumo wa Rais Mtendaji. Hii ilimaanisha kwamba Rais angelivaa 'kofia mbili': moja kama kiongozi wa nchi na nyingine kama kiongozi wa serikali.

Kulingana na muswada wenyewe, Rais angelichaguliwa moja kwa moja na wananchi; angeliongoza Baraza la Mawaziri aliowateua yeye; kungelikuwepo Makamu wa Rais aliyemteua yeye na ambaye angelikuwa kiongozi wa shughuli za serikali bungeni.

Kadhalika, Rais angeliteua majaji wa Mahakama Kuu na mabalozi wa kuliwakilisha taifa katika mataifa ya nje; makatibu wakuu wa wizara; mkuu wa jeshi; wakuu wa jeshi la polisi na magereza; wakuu wa wilaya na mikoa. Vile vile, Rais angelikuwa na madaraka ya kusaini au kutosaini muswada wowote katika sheria. Kama robo tatu ya wabunge wangeliupitisha tena muswada huo na kumtaka tena ausaini katika sheria, Rais angelilazimika kulivunja Bunge na kuitisha uchaguzi mpya.

Kulingana na makala aliyoyaandika Bwana Nyerere tarehe 3 Juni 1962 (siku 4 baada ya muswada kuwakilishwa bungeni) kwenye gazeti la *Observer* la nchini Uingereza, kwa kuwa Rais ndiye angelikuwa akiwateua hawa wote angeliweza, pale inapobidi, kusitisha ajira zao ingawaje kwa lengo la kudumisha 'nidhamu' katika Utumishi wa Umma. Aliendelea kufafanua kwamba, hata majaji wa Mahakama Kuu sharti wafahamu kuwa ingawa baada ya kuteuliwa wangelikuwa na usalama wa umiliki '...mtu anaye wateua ni Rais'.

Inaelekea ujumbe wake ulifika nyumbani. Lakini katika muktadha wa muswada wenyewe, tafsiri ya 'nidhamu' ilikuwa pana mno. Isitoshe, kulingana na Katiba ilyozungumziwa mwanzo (ambayo iliileta serikali ya T.A.N.U madarakani miezi 5 kabla ya muswada huo kupelekwa bungeni) watumishi wa umma hawakutakiwa waegemee upande wowote wa siasa.

Sababu yenyewe ni kwamba, kinyume na wanasiasa, watumishi wa taasisi hii huwa hawachaguliwi na mpiga kura bali huajiriwa na taifa. Kwa hiyo, kanuni hii ililenga kuwapambanua wanasiasa na watumishi wa umma.

Katika taifa linaloutumia mfumo wa demokrasia (kama Tanganyika ilivyokuwa wakati muswada huu ulipowakilishwa bungeni) wanasiasa hubadilika kila baada ya kipindi fulani, lakini watumishi wa umma hawabadiliki.

Ndiyo kusema, katika ujenzi wa taifa changa kama Tanganyika, utaalam pamoja na uzoefu wa watumishi hawa, ulikuwa mtaji mkubwa kwa taifa.

Mathlan, makatibu wa kudumu (walijulikana hivyo wakati huo) katika kila wizara, walikuwa ni nguzo imara ambapo kila waziri mpya aliegemea kutenda kazi yake kwa ufanisi. Kwa maana, hata waziri ingelikuwa ameelimika vipi, inawezekana kabisa asifahamu kila kitu katika wizara anayoiongoza—hata kama angelikuwa ameisha wahi kuwa waziri.

Kwa hiyo, kama serikali ya T.A.N.U ilitaka Utumishi wa Umma kuegemea upande wake, ingelikuwaje kama baadaye demokrasia ingeliileta serikali mpya madarakani? Je, walazimike kuegemea tena upande wa serikali mpya? Je, wangelimpaje huduma bila upendeleo, raia aliye ichagua serikali tofauti na ile wanayoishabikia?

Katika makala yaliyotajwa mwanzo (kwenye gazeti la *Observer*) Bwana Nyerere alisisitiza kwamba ilikuwa muhimu kufanya hivi ili '...Utumishi wa Umma uweze kushiriki kiamilifu katika mambo ya siasa ya taifa lao'.

Lakini watumishi wa umma walikuwa na haki kama raia yeyote kushiriki katika zoezi la kuwachagua wawakilishi wao na viongozi wengine wa kitaifa. Kulikuwa na wasiwasi ndani na nje ya nchi kwamba Katiba iliyokuwa ikipendekezwa na muswada ilikuwa ni ya kiimla.

Tarehe 2 Julai 1962, Bwana Nyerere alipokuwa mjini London akielekea Chuo Kikuu cha Edinburgh kutunukiwa shahada ya heshima ya Sheria (honorary Doctorate of Law), aliulizwa na waandishi wa habari kama Katiba iliyopendekezwa na muswada ingelikuwa ya kiimla. Alijibu kwamba haingekuwa kuwa hivyo kwa kuwa uimla ulikuwa ni 'mtazamo wa akili' tu.

Lakini baadhi ya Watanganyika mashuhuri kama Bwana Christopher Kassanga-Tumbo walidhani 'mtazamo' huo unaweza kujengwa na Katiba iliyopendekezwa na serikali. Mwezi mmoja baadaye Bwana Kassanga-Tumbo, ambaye wakati huo alikuwa balozi wa Tanganyika mjini London, aliachia wadhifa huo kuonyesha kutoridhika kwake na Katiba mpya.

Kama ilivyoonyeshwa awali mambo yalikuwa yakienda haraka kwani tarehe 28 Juni 1962, siku 27 tangu muswada kuwakilishwa bungeni, Bunge liliupitisha na kumpa Rais madaraka yote serikali iliyotaka apewe.

Lakini kikundi cha wabunge wa T.A.N.U kilichochaguliwa kuitunga Katiba mpya, maarufu kama 'constituent assembly', hakiwahusisha wananchi; vikundi mbalimbali kutoka jamii au wawakilishi kutoka kambi ya upinzani.

Tarehe 27 Septemba 1962 Bunge lilipitisha sheria ya watu kuwekwa kizuizini kwa muda usiojulikana kwa amri ya Rais.

Katika hatua hii, Bwana Christopher Kassanga-Tumbo, ambaye mara baada ya kuachia wadhifa wake aliunda chama cha ushindani cha People's Democratic Party, alichukuliwa mshikemshike na kuwekwa kizuizini kwa amri ya Bwana Nyerere.

Lakini Bwana Victor Mkello, kiongozi wa chama cha Tanganyika Federation of Labour na Katibu Mkuu wa Plantation Workers' Union pamoja na afisa mwenzake mwandamizi walipelekwa Sumbawanga, tarehe 7 Januari 1963, ambako walikaa kwenye kizuio.

Mapema, marehemu Chifu David Kidaha Makwaia OBE, wa Usiha, mkoani Shinyanga, alipelekwa kwenye kizuio wilayani Tunduru. Chifu Kidaha na Bwana Nyerere walikuwa marafiki tangu walipokuwa wote Makerere.

Kulingana na gazeti la *The Times* mjini London la tarehe 11 Mei 2007, Bwana Nyerere alipoanzisha T.A.N.U, Chifu Kidaha aliwashawishi machifu 50 waliokuwa chini yake kuiunga mkono T.A.N.U; na kweli walifanya hivyo bila kusita.

Lakini baada ya kuchukua madaraka hatua ya kwanza ya Bwana Nyerere ilikuwa ni kufuta uchifu na kumwekea kizuio Chifu Kidaha na kaka yake Hussein, lakini bila kueleza sababu ya kufanya hivi. Hawa ni baadhi tu ya viongozi mashuri walioanza kuwafagilia njia wazuiwa wengine, kama itakavyoonekana baadaye kwenye simulizi hii.

Tarehe 14 Januari 1963 alipokuwa akikifungua kikao cha mwaka cha wajumbe wa T.A.N.U, Bwana Nyerere alitangaza kwamba Kamati ya Utendaji ya chama ilikuwa ikilitaka Bunge kupitisha sheria ambayo ingelitambua Tanganyika kama taifa la chama kimoja (T.A.N.U).

Aliendelea kusema kwamba kwa kuwa chama cha T.A.N.U kilikuwa na wafuasi wengi nchini, ilimaanisha kwamba wananchi hawakuwa na haja ya mfumo waliouridhi wa vyama vingi.

Inaelekea tafsiri hii haikuwa sahihi, kwa maana mpiga kura asingelivutiwa na sera za T.A.N.U (ambazo hazikuhusisha kuangusha Katiba ya nchi au kuvipiga vyama vingine marufuku) kama havikuwepo vyama vingine kulinganisha. Ilikuwa dhahiri katika hatua hii kwamba 'mtazamo wa akili' ulikuwa kazini ukiweka msumari wa mwisho kwenye jeneza la mfumo wa vyama vingi vya kisiasa.

Ni wazi pia kwamba haikuwa vigumu serikali kuitekeleza azma hiyo kwa sababu Katiba ya kidemokrasia ya 1961—1962 ilikwisha tupwa kapuni, siku ambayo wabunge wa chama cha T.A.N.U walipopitisha muswada wa Katiba mpya (28 Juni 1962).

Lakini utata ulioibuliwa na matukio haya yote utaendelea kubaki kwenye vichwa vya Watanzania wa leo na kesho: ni kipi muhimu, Katiba yenyewe au **heshima** na **nguvu za kisheria** inazopewa Katiba hiyo na wanaoiendesha?

****

•Itaendelea na **Mfumo Mpya: Chama Kimoja 'Kushika Hatamu'**

****

REJEA

Barabara ya Tanzania Kwenda Damascus

ALLEN, G. (1964) Africa's Freedom, UNWIN BOOKS, London, United Kingdom

OTHMAN, H. (14.10. 2005) Mwalimu Julius Nyerere: An Intellectual in Power, a Memorial Lecture, in Commemoration of the 6th Anniversary of Mwalimu Julius Nyerere's death, Organised by the East ASfrican Students Society.

SEGAL, R. (1962) African Profiles, PENGUIN AFRICAN LIBRARY, London, United Kingdom.